



MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA DAR ES SALAAM

MAELEZO MAFUPI YA MRADI WA MBAGALA MAJIMATITU SHULE YA MSINGI A NA MAJIMATITU KWA LUMBANGA

UTANGULIZI

Ujenzi wa mradi wa maji katika Shule ya Majimatitu ulifanyika baada ya kuonekana kwamba kuna upungufu mkubwa kubwa wa maji safi na salama katika shule hiyo. Hali hii ilichangiwa na kuwepo idadi kubwa ya wanafunzi baada ya serikali kutangaza kuwa elimu ya msingi ni ya bure. Hivyo Mkoa kwa kushirikiana na DAWASA walipendekeza kutafutwe chanzo cha maji ya kutosha kuweza kuwahudumia wanafunzi wote.

MATOKEO YA UCHIMBAJI WA VISIMA

Visima viwili vilichimbwa na Wakala wa serikali wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (DDCA) kwa gharama ya **Tsh. 24,500,000**. Kisima cha maji katika shule ya Msingi Majimatitu kina urefu mita 142 na uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita 7,200 kwa saa. Kisima cha Majimatitu kwa Lumbanga kina urefu wa mita 132 na uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita 6,600 kwa saa.

UJENZI MIUNDOMBINU

DAWASA iliajiri mjenzi wa mradi, Kampuni ya M/S Bota Construction Ltd. Gharama ya ujenzi wa mradi kulingana na Mkataba ni kiasi cha **Tsh 94,861,585.00** na muda wa mkataba ilikuwa ni siku 120. DAWASA ililipia gharama ya uunganishaji wa umeme TANESCO kwa **Tsh 4,800,000**. Ujenzi wa mradi lianza mwezi wa 10 mwaka 2016 na ulikamilika mwezi Februari mwaka 2017. Mkataba

wa ujenzi ulijumuisha;

- I) Ujenzi wa minara miwili (2) yenye urefu wa mita sita na nusu,
- II) Uwekaji wa mataki mawil ya maji yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha lita 10,000 kila moja,
- III) Usambazaji wa mabaomba na
- IV) Ufungaji wa pampu katika kila kisima. Pampu zilizofungwa zina uwezo wa kujaza maji kwenye tanki kwa muda wa lisaa limoja na nusu.

HALI YA MRADI

Kwa sasa mradi ulikamilika na kukabidhiwa kwa Manispaa ya Temeke/ shule wakati wa wiki ya maji Machi 2017 baada ya kuzinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda. Miradi hii inawanufaisha wanafunzi pamoja na wananchi waliopo jirani kuweza kupata majisafi na salama. Aidha kutokana na wingi wa wananfunzi katika shule mradi utasaidia katika maswala ya usafi na kuepuka magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya maji yasiyo salama.